

101/2

KISWAHILI

Karatasi Ya 1

INSHA

DISEMBA 2021

Muda:Saa 1 ¾

MTIHANI WA PAMOJA WA MOMALICHE 4

MSURURU WA 8

Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

1. Andika barua kwa mhariri wa gazeti la sauti ya mzalendo kuhusu madhara ya janga la korona nchini Kenya.

✓ Mwanafunzi azingatie muundo wa barua kwa mhariri kikamilifu.

Madhara ya janga la korona nchini Kenya.

- Kukatizwa kwa elimu
- Vifo
- Kufutwa kazi
- Kudorora kwa uchumi
- Ndoa za mapema
- Mimba za mapema
- Gharama kubwa ya matibabu
- Woga mionganini mwa wananchi
- Kudorora kwa mila na tamaduni za jamii.

(Mwalimu akadirie maudhui ya wanafunzi)

2. Vyama vya wanafunzi shuleni vina manufaa ya kuhusudiwa.Jadili.

Manufaa ya vyama vya wanafunzi shuleni.

- Hukuza vipawa na kuimarisha stadi za kujieleza
- Huhimiza utangamano mionganini mwa wanachama
- Husaidia mwanafunzi kukabiliana na changamoto za maisha
- Humfunza mwanafunzi maadili ya kijamii na kidini
- Majukumu ambayo mwanafunzi hupewa hupalilia uwajibikaji,uaminifu na kipawa cha uongozi
- Kupitia vyama hivi mwanafunzi anaweza kuwahamasisha wenzake dhidi ya tabia hasi k.v mapenzi ya kiholela n.k
- Shughuli na miradi ya vyama hivi humwezesha mwanafunzi kutumia nishati zake kwa njia ya kunufaisha na kuepuka maovu.
- Vyama vya michezo humwezesha mwanafunzi kuimarisha afya na kujenga misuli.

- Vyama vya michezo huweza pia kuwa msingi wa kupata chanzo cha riziki baadaye.
- Vyama vya wanafunzi ni msingi wa mshikamano na maridhiano.
(Mwalimu akadirie maudhui ya wanafunzi.)

3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo.

Mwenye kovu sidhani kapona.

- ✓ Msimulizi asimulie kisa kitakachoonyesha ukweli wa methali hii.
- ✓ Maana-Mtu ambaye amewahi kuwa mbaya hata akionekana kubadili mwenendo huenda akarudia maovu yake.
- ✓ Mtahiniwa aonyeshe:
 - a) Makosa ambayo mhusika alifanya.
 - b) Jinsi makosa hayo yalimfanya kubadili mwenendo wake.
 - c) Kurudia makosa yale au mengine mabaya zaidi.
- ✓ Kisa ndicho muhimu si utangulizi

4. Tunga kisa cha kusisimua na kumalizika kwahivyo ndivyo ukurasa mpya katika kitabu cha maisha yangu ulivyofunguka.

- ✓ Mtahiniwa asimulie kisa kitakachoonyesha mabadiliko yaliyotokea katika maisha yake.mabadiliko haya yaweza kuwa mazuri au mabaya.
- ✓ Mtahiniwa atumie wakati uliopita ; aonyeshe matukio yaliyomfikisha katika mabadiliko haya.
- ✓ Kisa kioane na mdokezo aliopewa.

maudhui yasipungue $6 \times 2 = 12$

Muundo –alama 4

Lugha -4